**Petro Kime Risase, (1890 – 1982)**

Petro Kime Risase alikuwa mwalimu na mmishonari mtangulizi mzawa katika Afrika Mashariki.

**Miaka ya Awali**

Petro Kime Risase alizaliwa kati ya 1888 na 1891 katika Kijiji cha Kihurio, Milima ya Pare Kusini, Wilaya ya Same, Mkoa wa Kilimanjaro nchini Tanzania. Wazazi wa Petro walikuwa Mzee Kime Risase na mama yake. Kime Risase aliishi katika kijiji alikozaliwa, alikotumia muda mwingi wa utoto wake. Wazazi wake walikuwa wapiganaji dhidi ya Wamasai waliokuwa wakiwaiba mifugo. Wazazi walimfundisha Petro kufanya kazi kwa bidii na pia walimshawishi awe mmishionari.

Wazazi wake waliishi Kihurio – Mareti, na baba yake alikuwa mtengeneza vitanda katika jumuiya hii yenye kujishughulisha sana na shughuli nyingi za kiuchumi iliyokuwa kwenye njia ya zamani ya msafara wa watumwa chini ya Milima ya Pare. Waadventista wa Sabato walipofungua misheni huko Kihurio mwaka 1905, kilichokuwa kituo chao cha pili hapa nchini, alikuwa miongoni mwa wanafunzi wa kwanza kuhudhuria shule yao. Wakati huohuo, alitumika kama mhudumu wa mmishionari Ernst Kotz na baada ya muda mfupi pia alifanya kazi kama msaidizi wake wa lugha na utafsiri. Risase alibatizwa mwaka 1909 huko Mamba-Giti (wakati huo ikiitwa Friedenstal Mission Station, kituo cha kwanza cha Waadventista kilichoanzishwa Tanzania mwaka 1903). Dada yake Rebekka aliolewa na Petro Mlungwana, mwongofu mwingine wa mapema na kiongozi wa kanisa la Pare wa kizazi cha kwanza.

**Elimu**

Petro alikuwa na umri wa miaka 12 wakati wamishionari wa Kijerumani wa Kiadventista walipofika Kihurio. Alipokuwa akifanya kazi katika nyumba ya Ernst Kotz, Petro alifanya majukumu kadhaa ikiwa ni pamoja na kuchapa na kutumika kama msaidizi wa lugha na tafsiri, jambo ambalo lilimpa nafasi nzuri ya kusoma na kujifunza neno la Mungu. Risase alibatizwa mwaka wa 1907 huko Mamba – Giti, wakati huo ikiitwa Friedensatal Mission Station, kituo cha kwanza cha misheni cha Waadventista kilichoanzishwa nchini Tanzania mwaka 1903 na wamisionari wa Kijerumani, EC Enns na Johannes Ehlers.

“Nilipokuwa mtoto wa miaka kumi na miwili hivi”, Petro anasimulia, “wamishionari wa Kijerumani wa kanisa la SDA walifika katika nchi yangu na kuanza kufungua shule zipatazo 1,902. Nilienda shule kwa muda lakini punde si punde nilipewa kazi na wamishionari hao ya kuwa mtumishi wa ndani, na wakati huo huo nikiendelea kujifunza kusoma. Kisha nikaingia katika darasa la ubatizo, na kubatizwa mwaka wa 1907.”

Risase alimaliza shule ya msingi mwaka 1910 baada ya hapo alifanywa kuwa mwalimu. “Sisi vijana wawili tulitumwa mahali ambapo hapakuwa na Wakristo, kufundisha shule na kuhubiri ujumbe,” Risase anakumbuka kuwa kama matokeo ya bidii yake kazini, wamishionari walikwenda huko na kujenga kituo cha misheni na kuwabatiza waumini wapya. Petro Risase alisaidia wamishionari kutafsiri Agano Jipya

katika lugha ya Kipare. Mnamo 1912, Petro alimuoa Mary, binti wa Chifu Kantu ambaye pia aliishi Kihurio. Harusi yao ilifungwa katika Kanisa la Kihurio wilaya ya Same, na mkoa wa Kilimanjaro. Mary alijifungua mtoto wa kike aliyeitwa Anna, lakini kwa masikitiko, mama na mtoto walikufa mara tu baada ya kujifungua.

Mnamo 1914, Petro alihamishiwa misheni ya huko Kihurio kufundisha katika shule ambayo hapo awali alikuwa mwanafunzi. Mnamo 1919, Risase alimuoa Naetwe, ambaye alimzaa Gadi, Monica, Gideon, Orgenes na Silas. Naetwe aliishi maisha yake yote na mumewe hadi alipoaga dunia mapema mwaka wa 1960.

**Uchungaji**

Vita vya Kwanza vya Dunia vilipoanza mwaka wa 1914, Risase aliacha kufundisha ili kusaidia kukamilisha tafsiri ya Agano Jipya haraka iwezekanavyo. Alifanya kazi hii kwa uaminifu kwa muda wa mwaka mmoja na akamaliza kazi hii mwaka wa 1915. Kisha akaendelea kufundisha hadi 1917 wakati wamishionari wote wa Kijerumani walipoondoka eneo la Tanganyika. Miaka mitatu baadaye, wamishonari Waingereza walikuja kuchukua nafasi hiyo ya Wajerumani. Hata hivyo, kazi ya shule kwa ule utaratibu wa kawaida ilikoma. Katika kipindi hiki, Petro Risase aliendelea kuwafundisha watoto wa Wakristo wa SDA bila malipo yatokanayo na ajira. "Nililazimika kufanya kazi bila malipo" anadokeza Petro Risase. Mchungaji Spencer Maxwell alipokuja kusimamia kazi katika Tanganyika Mashariki, walimu ambao walikuwa wamebaki wakifanya kazi wakati wa Vita vya Kwanza vya Dunia walilazimika kuacha kufanya kazi hadi waliporudishwa tena. Kwa hiyo, ilimbidi Petro kufundisha katika shule mbalimbali hadi mwanzoni mwa 1926 alipoitwa kufanya kazi ya uinjilisti.

**Atumwa Uganda**

Mwaka 1927 Mchungaji Spencer Maxwell alipoondoka Tanganyika kwenda kufungua kazi Uganda, Risase alitumwa kuandamana naye. “Mwaka wa kwanza nilikaa na Mchungaji Maxwell katika kituo cha misheni cha Nchwanga; kisha nikatumwa sehemu nyingine ya Uganda kufungua kazi. Nilipoondoka mahali pale mnamo 1931 kulikuwa na washiriki wapatao kumi na watano waliobatizwa huko, wanne kati yao tayari walikuwa wameanza kufanya kazi kwa ajili ya misheni yetu kama walimu.”

**Arudi nyumbani**

Mnamo 1931, Petro alipewa likizo ya miezi minne kutembelea watu wake huko Pare, Tanganyika. Aliporudi Uganda, alitumwa Kampala kufanya kazi na Mmishionari Valdemar Toppenberg. Kazi yake pamoja na wamishionari wengine huko Kampala iligeuka kuwa ngumu sana; hata hivyo, walifanikiwa zaidi katika vijiji vya nje ya mji wa Kampala ambapo walianzisha kanisa la waumini kumi na tisa. Akiwa Uganda, alifanya kazi pamoja na wamishionari wenzake wa Pare Abrahamu na Raheli Msangi kuanzia 1928 hadi 1931.

**Kuwekewa mikono ya uchungaji**

Mnamo 1934, Petro Risase aliwekewa mikono ya kichungaji kwa huduma ya Injili kama Mtanzania wa tatu kutawazwa kuwa mchungaji katika Kanisa la SDA. Alikuwa

Mtanzania wa tatu kutawazwa kuwa mchungaji katika Kanisa la Waadventista Wasabato na alikuwa kiongozi muhimu wa kiroho miongoni mwa Waadventista Tanzania, Uganda na Kenya. Mapema mwaka wa (1934) alipewa likizo nyingine mwishoni na akahamishiwa Kenya kufanya kazi katika eneo la Mombasa, eneo la Waislamu.

**Kazi zake akiwa Mombasa**

Akiwa Mombasa alifungua misheni ya Waadventista huko Changamwe, umbali kidogo kutoka kisiwa cha Mombasa. Petro Risase akishirikiana na Mmishionari WC Raitt, walianzisha makundi ya Chonyi, Paziani, na Singwaya na kubatiza watu wengi. Hata akiwa huko Mombasa, Risase hakusahau kuwatembelea jamaa zake huko Upareni ingawa walikuwa mbali sana na waliishi nje ya nchi.

Mchungaji Petro Risase alipokuwa Mombasa, alitembelea jamaa zake mara kwa mara huko Kihurio kwa kuendesha baiskeli kutoka Mombasa kupitia Tanga. Alipokuwa akiwatembelea wapendwa wake huko Kihurio, aliendа na aina mbalimbali za vitu vya ukumbusho kutoka Mombasa ikiwa ni pamoja na miche ya matunda na miti mbalimbali kwa ajili ya kupanda katika nyumba za ndugu zake. Hivi sasa miti hiyo ya matunda imeenea sana katika Kijiji cha Kihurio cha sasa.

**Baada ya Vita ya pili ya dunia**

Ushahidi wake wenye nguvu zaidi ulitokea wakati walimu wa Tanganyika walipofungwa gerezani kipindi cha Vita vya Pili vya Dunia. Walimu waliambiwa wangeendelea kufungwa hadi vita viishe. “Wakati huo, (katikati ya Oktoba) tuliomba kwa bidii sana, tukiwafikiria wafuasi wetu waliokuwa vijijini, ili kwamba ikiwa kweli hii ni kazi ya Mungu, basi awaongoze viongozi watuachie huru Novemba 1, twende nyumbani kuwaangalia waumini.” Alisema Risase. “Afisa aliyetufunga alikuwa Mkatoliki na hakutupenda.”

Karibu na mwisho wa Oktoba, walianza kuogopa kwa vile hawakuwa wamepokea jibu lolote kuhusu ombi lao, na sasa waliwekwa chini ya uangalizi mkali sana. Hata hivyo, mwishowe Mungu aliingilia kati, na wakaachiliwa. Mara tu waliporudi nyumbani, walikusanyika pamoja tena, wakamshukuru Mungu kwa kujibu maombi, na kuahidi kumfanyia Mungu kazi daima iwe wameajiriwa na misheni au la. “Tangu utoto wangu sikupenda kutoka nyumbani, lakini kutokana na ahadi hii siku zote nimekuwa tayari kwenda mbali kwa ajili ya misheni, hata Uganda nilipoitwa huko. Kwa sababu ya uzoefu huu ninatamani kukaa katika kazi ya Mungu maisha yangu yote.” Anasema Petro.

**Miaka ya Baadaye**

Petro Risase alistaafu utumishi wa kuajiriwa na kanisa huko Kihurio mnamo Desemba 31, 1947, na baada ya kustaafu aliendelea na kazi ya kanisa kwa kutoa semina kwa waumini wa kanisa hilo, kufunga ndoa, na kufanya ubatizo katika maeneo mbalimbali ya Kaskazini Mashariki mwa Tanzania. Alikuwa ametambuliwa kwa kazi yake ya umishionari katika Afrika Mashariki. Petro Risase alifariki dunia Desemba 7, 1982,

kwenye Misheni ya Kihurio, Wilaya ya Same nchini Tanzania, na akazikwa huko na kuacha watoto wake watatu.

**Urithi aliotuachia**

Maisha ya Petro Risase yalikuwa na matokeo muhimu sana kwa Kanisa la SDA kwa kuwa kazi yake ya kutafsiri Agano Jipya katika lugha ya kienyeji ya Wapare ilipelekea kuenea kwa haraka kwa Injili katika milima ya Pare na Tanzania kwa ujumla. Hii ilisababisha kuanzishwa kwa kanisa la kwanza la SDA katika Afrika Mashariki na taasisi za elimu za kanisa kama vile Shule ya Sekondari ya Suji, Shule ya Sekondari ya Parane, na nyinginezo.

Mchango wa Petro Risase katika Konferensi ya Kaskazini Mashariki mwa Tanzania hasa ulihusisha kuongeza shauku miongoni mwa washiriki wa kanisa kujua jinsi ya kusoma Biblia ya Kipare na kuwahimiza washiriki kwenda shule. Huwezi kutaja Kanisa la SDA katika Milima ya Upare bila kutaja jina la Petro Risase.

Pia Petro Risase anasifiwa kwa kuinua moyo wa umishionari katika Afrika Mashariki kwa sababu ya kufanya kazi nchini Tanzania, Uganda, na Kenya. Aliwashawishi vijana wengi wa kiume na wa kike, wazee na vijana kuwa na shauku ya kufanya kazi kama wamishionari. Alikuwa mfano wa kuigwa katika kazi ya umishionari. Petro Risase alipokuwa anarudi kutoka Uganda na Kenya baada ya muda wake wa wito, watu wengi walikuwa wakimuuliza kuhusu kazi ya umishionari, na wengine wakitaka kuungana naye huko. Baadhi ya watu waliamua kumheshimu kwa kushiriki pia katika kazi ya umishionari aliyokuwa akiifanya katika Fildi ya Kaskazini Mashariki mwa Tanzania.